

TANGAZO LA SERIKALI Na. 300 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURAYA 355)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ISAKALILO YA
MWAKA 2023

- Jina
1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Isakalilo ya mwaka 2023.
- Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355
2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.
- Mipangokina ya eneo
3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

—
JEDWALI
—

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira – nukta 791917MS, 9138107KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira- nukta 792452MS, 9136967KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira- nukta 792750MS, 9136528KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira- nukta 787698MS, 9132627KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 2.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira –nukta 785994MS, 9134462KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 786505MS, 9135995KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 3.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P7 yenye majira - nukta 788959MS, 9135676KZ; baada ya hapo unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P8 yenyemajira -nukta 789701MS, 9136518KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P9 yenye majira - nukta 791366MS, 9137379KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi*